Archdiocese of Arusha
wasso hospital

03/2/2026

# TANGAZO LA KAZI

## HOSPITALI YA WASSO – JIMBO KUU KATOLIKI ARUSHA

## WILAYA YA NGORONGORO

Hospitali ya Wasso ni hospitali ya kanisa jimbo kuu katoliki la Arusha inayotoa huduma za afya kwa jamii ya Ngorongoro na maeneo ya jirani.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wasso anakaribisha maombi ya kazi kwa kada ya **Daktari Daraja la II.**

1. **DAKTARI DARAJA LA II (MEDICAL DOCTOR II)** NAFASI (1)

### a) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Shahada ya Udaktari (MEDICAL DOCTOR)
- Awe amesajiliwa na Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika – MCT).
- Awe na leseni halali ya kufanya kazi.
- Awe na uzoefu wa kazi (uzoefu utazingatiwa )
- Awe na maadili mema, bidii, na uwezo wa kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine.

### b) MAJUKUMU YA KAZI

- Kutoa huduma za uchunguzi na matibabu sahihi kwa wagonjwa.
- Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya wagonjwa.
- Kushirikiana na timu ya wahudumu wa afya kuboresha huduma.
- Kutunza kumbukumbu sahihi za wagonjwa.

### MASHARITI YA JUMLA

i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI.
iii. Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura.
iv. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
v. **Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, hati ya matokeo ya kidado cha nne na sita (FORM IV AND VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
vi. **Mwombaji aliyesoma nje ya Tanzania ahakikishe cheti chake kimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**

vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi mhusika atachukuliwa hatua za kisheria.

**viii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 28 February, 2026.**

**ix. Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wasso S. L.P. 42, LOLIONDO, barua pepe. secretary@wassohospital.org.**

..............................

Angela Joseph
**Kny: MGANGA MFAWIDHI**

WASSO HOSPITAL
P.O. Box 42
LOLIONDO
ARCHDIOCESE OF ARUSHA